# *Kwa Nini?*

. . .?. . . Asante.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunapokikaribia kiti Chako cha neema usiku wa leo, tunakuja katika Jina hilo linalojitosheleza kwa yote la Bwana Yesu pamoja na hakikisho lililobarikiwa, ambalo Yeye ametupatia, kwamba tungesikiwa, na maombi yetu yangeshughulikiwa. Tungeomba kwanza msamaha wa dhambi zetu na dhambi za watu. Nasi tungeomba tena ya kwamba baraka Zako zitaendelea kujulikana miongoni mwetu, kusudi Jina Lako lipate kuheshimiwa.

3 Bariki maneno yanayosemwa katika wimbo na mahubiri pia, ushuhuda, ama chochote kinachoweza kufanywa. Waponye wagonjwa, waokoe waliopotea, wape Roho Mtakatifu wale walio na njaa na kiu. Na jalia huu uwe usiku wa kukumbukwa kwa sababu ya Uwepo Wako. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

4 Mwaweza kuketi. Nilikuwa nikisema hivi majuzi asubuhi kwenye kiamshakinywa, "Sikuzote mimi huchelewa kidogo tu." Nami nilikuwa nikihubiri kwenye kanisa la United Brethren si muda mrefu uliopita, nami nilikuwa, niliingia, yapata saa moja nimechelewa na kwa hiyo mhudumu akasema, "Sasa nitamtambulisha mchelewaji [Katika Kiingereza "the late" maana yake marehemu—Mfa.] Bw. Branham."

5 Nikasema, "Vema, sikuzote nimechelewa kidogo. Mama yangu alisema nilikuwa mtoto wa miezi tisa kamili, basi ilionekana kana kwamba sikuwa na wakati wa kutosha, nilikuwa na uzito wa ratili tano tu. Kisha nilipooa, mimi . . . mke aliningojea kwa karibu saa moja. Nilikicheleweshа kitu hicho chote mpaka nilipowatembelea wagonjwa hospitalini na kurudi. Na laiti ningechelewa kwenye mazishi yangu sasa, hilo ndilo jambo linalofuata, kama ninaweza tu kuyaahirisha hayo kwa muda sasa, sitaki hayo yaje upesi sana, kwa hiyo, ninataka kukaa na kumtumikia Bwana."

6 Ni vema kuwa hapa na kuwa na kusanyiko hili zuri la watu tena, usiku wa leo. Nafikiri asubuhi, kwenu ninyi mnaoishi karibu na Los Angeles, kuna kiamshakinywa cha Wafanyabiashara Wakristo asubuhi. Ninaamini wangali wanakiandalia kwenye Mkahawa wa Clifton, nami natumaini kuwa huko asubuhi.

7 Nimesikia ya kwamba Ndugu Shakarian amekuwa mgonjwa sana. [Ndugu fulani anasema, "Atakuweko."—Mh.] Atakuweko? Vema, hilo ni jema. Ndugu Demos Shakarian,

ndu—ndugu wa binafsi, rafiki msiri wangu. Ninasikitika kusikia habari zake. Nilisikia alikuwa mgonjwa kidogo, bali sikujua alikuwa mgonjwa kama vile alivyokuwa, alidhoofika tu kabisa. Nilimwambia yapata miaka miwili iliyopita afadhali apumzike kidogo tu, akaangalia nyuma, kasema, "Tekeleza yale unayohubiri." Na kwa hiyo . . .

8 Ninakumbuka mara ya mwisho hapa, wakati Raymond Richey aliponishika kwa mguu wa suruali tulipokuwa tukija kanisani huku chini Los Angeles, la, samahani, huko Long Beach, tulikuwa tukiingia kwenye hilo jumba la mikutano kule usiku huo. Naye Raymond ni rafiki msiri wangu, naye alikuwa amevurugika, alikuwa katika hali mbaya sana. Naye akasema, "Ndugu Branham, usiende kwa muda mrefu sana." Ndio kwanza arudi kutoka Korea. Raymond, amekula chumvi nyingi pia, mwajua. Akasema, "Utajiua." Kisha kasema basi, "Angalia hali niliyomo sasa."

9 Nami nimekuwa katika hali hizo, kwa hiyo ninajua ni nini. Nami ninaona mengi sana ya kufanywa, hata hivyo wewe . . . inaonekana kana kwamba huna wakati wa kuyafanya, na inakutia wasiwasi. Kwa hiyo ninatumaini tu Bwana atanisamehe, kwamba bidii yangu haitashinda hekima yangu, Yeye alinipa hekima kujua jinsi ya kushughulikia bidii yangu, hasa.

10 Ni vema kuwa hapa, usiku wa leo, pamoja nanyi ndugu pia, huku nyuma, kwenye wakati huu, Les Kopp na ninyi nyote ndugu. Wazuri sana, wasikilizaji hawa wazuri hapa, nina furaha sana kuona ninii . . . mikutano hii, inaonekana kama kila mtu katika moyo mmoja na nia moja, inaonekana kana kwamba lolote lingeweza kutukia. Nayo mikutano michache iliyopita imekuwa hivyo, nami ninamshukuru sana Bwana.

11 Mradi tu inaendelea hivyo najisikia kuwa ninaweza kuendelea tu mbele kidogo. Wakati . . . Ni wakati unapofikia mizozo hiyo, hapo ndipo huwa mbaya, unajua, na—na hakuna umoja, na, lakini hapa imekuwa tu ni udugu mmoja mkubwa mno. Kila kitu, tunashukuru sana kwa ajili ya hilo, Bwana na aendelee.

12 Sasa, tunatambua ya kwamba hatuna mapambo juu ya mikutano tuliyofanya mara ya kwanza. Kwa kawaida uamsho hutokea, unadumu, kulingana na historia, yapata miaka mitatu. Kwa kawaida mhudumu hutoa kilicho bora sana katika miaka mitatu, baada ya hapo anaishi kwa sifa yake ya kile alichotengeneza katika miaka hiyo mitatu. Nina furaha sana niliweka zangu juu ya Neno. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo ninaweza kuishi kwa Neno.

13 Ninaamini tu Biblia hii ya kale iliyobarikiwa, nafikiri tu ndiyo Kitu adhimu kuliko vyote, nami nafikiri ya kwamba Hiyo—Hiyo ni Mungu. Neno ni Mungu katika maandishi. Na

wakati Roho Mtakatifu anaposimama juu Yake, Yeye hulifanya tu Hai.

14 Nilikuwa nikizungumza na mtu fulani. . .Tuna mahojiano ya faragha, na hapo ndipo inakubidi. . .Sisi. . .Jambo lingine, nyumbani nafikiri kulikuwa na mia tatu kwenye orodha tulipoondoka, wakingojea mahojiano hayo ya faraghani. Tunaingia pamoja na watu, tunafunga tu mapazia, nasi tunakaa mle mpaka, tunaomba mpaka Bwana afunue kwa ono jambo la kufanya. Sasa, tunajua Neno la Bwana linatwambia, na linaweka huo mpango, lakini wakati mwingine kuna mambo maishani mwa mtu ambayo hawajui la kufanya. Na hapo ndipo tunapokaa mbele za Bwana mpaka litakapojibiwa. Halafu tunayafikia mahojiano haya, kama vile tulivyokuja huku, watu katika wilaya hii huenda wamekuwa wakingojea, baadhi yao, kwa miaka minne au mitano kwa ajili ya mahojiano haya.

15 Basi tulikuwa tukizungumza, naamini ilikuwa ni jana, ama asubuhi ya leo, mojawapo, kuhusu Nuru inayoangaza katika siku za mwisho. Sasa, nimejiepusha na kuhubiri, kwa sababu niko tu hapa kuwaombea wagonjwa, na kutupa wavu wangu pamoja na ndugu zangu na kuvuta. Lakini kwa kweli ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, ni moja kwa moja katika wakati wa mwisho.

16 Nami ningetaka kuchukua ku—kundi kama hili, umoja wa roho na moyo, na laiti tungalikuwa na yapata—yapata majuma mawili au matatu ambapo tungeanza tu, kufanya ibada za alasiri, na ibada za asubuhi, na ibada za jioni, na kuileta tu Biblia tunavyoiona.

17 Nami nimeshukuru sana. Yupo msomi wa Kiyunani anayeketi nyuma yangu, nami nilikuwa pamoja naye hivi majuzi. Mtu huyu anatoka Ugiriki, baba yake ni mhudumu mashuhuri huko Ugiriki, naye huchukua kanda zangu. Naye akasema, "Ndugu Branham, nilifikiri wewe ni msomi wa Kiyunani."

Nikasema, "Hata sijui Kiingereza kizuri, acha hata neno moja la Kiyunani."

18 Akasema, "Lakini nikileta nomino zako, viwakilishi nafsi, na kila kitu katika mafundisho yako kwenye kanda zako," kasema, "Ninaweza kuweka mstari namna *hii* nayo yatagawanyika kikamilifu na kufanana moja kwa moja na Kiyunani."

19 Nami nikasema, "Vema, ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo, kwa sababu daima mimi hujaribu kujisikia nikiongozwa na Roho Mtakatifu kusema yale ninayosema. Nayo. . . Mimi. . .Kama alisema jambo lolote kinyume na Biblia, basi nisingeliamini, mnaona, nisingeamini ya kwamba ilikuwa ni Roho Mtakatifu, kwa sababu daima atadumu katika Biblia, Roho Mtakatifu atadumu."

20 Nasi tulikuwa tukizungumza juu ya maskini mwanamke huyu niliyekuwa, alasiri ya leo, asubuhi ya leo, ninaamini ndivyo, ambaye tulikuwa tukizungumza juu ya maskini mwanamke yule niliyenena habari zake, maskini jamaa huyo mwenye sifa mbaya aliyekuja kisimani huko Sikari, naye akamwona Bwana Yesu, wala hakumtambua, hata hivyo alikuwa awe mmoja wa wanafunzi Wake.

21 Sasa, nina Fundisho dogo la kigeni, na sasa, kama haliendani na lenu, fanya vile vile nifanyavyo ninapokula kuku wa kukaanga nyumbani kwako, kweli ninapenda kuku wa kukaanga, na ninapoufikia mfupa, siachi kula kuku, ninatupa tu huo mfupa, na kuendelea kula kuku. Kwa hiyo sasa, ninyi amininі jambo lile lile.

22 Sasa, ninaamini ya kwamba jina la Kanisa liliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati, kabla ya Mwana-Kondoo kuchinjwa, maana Biblia ilisema mpinga-Kristo angewadanganya wote walio juu ya nchi ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ninaamini Mungu asiye na kikomo, kwa kujua Kwake tangu zamani, aliliona Kanisa.

23 Sasa, ninajua hilo ni somo gumu, na kumbukeni, kuna ukweli kwake, siliamini kama wengi wanavyoliamini, lakini ninaamini ya kwamba kunao, kwa kujua kimbele Mungu angeweza kujua mwisho tangu mwanzo, maana Yeye ni Mungu asiye na kikomo. Sasa, kama mimi ni sehemu ya Kanisa hilo, natumaini ndivyo nilivyo, ninautafuta tu wokovu wangu mwenyewe kwa hofu na kutetemeka, nikidumu moja kwa moja katika Neno. Ambapo, kama nikitoka Mle, basi nitaomba kurudi ndani Yake tena.

24 Na kwa hiyo wakati hilo, si neno zuri kutumia, mnaona, lakini wakati Mbegu hiyo iliyochaguliwa tangu zamani iliyokaa ndani ya maskini mwanamke huyo, akiamini, akiangalia, hata hivyo katika hali yake ya dhambi, alikuwa akitazamia kuja kwa Masihi. Utaratibu wa kanisa katika siku hiyo ulikuwa hivyo, karibu kama ulivyo leo. A—angeweza kuishi kama tu alivyokuwa akiishi, na, hakika aliona dhihaka ya jinsi watu waliokiri kuwa wa kidini na hawakuwa kitu ila lundo la unafiki. Nami nasema hivyo si kwa kukufuru, nasema hivyo kwa uaminifu, na mwaminifu moyoni mwangu, na upendo kwa kila mtu.

25 Halafu basi, wakati hiyo . . . wakati . . . Alikuwa amesimama pale akingojea kuona jibu la Mtu huyo lilikuwa nini aliposema, “Si kawaida,” alikuwa akiingia katika mapokeo wakati huo, ya wazee, “kwenu Wayahudi kumwomba Msamaria, mimi, mwanamke Msamaria ki—kitu kama hicho, ama kuwa na shughuli zozote.”

26 Akasema, "Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe." Ndipo swali likazuka, naye Yesu akasema, "Nenda, kamwite mumeo."

Akasema, "Sina."

27 Akasema, "Vema umesema, kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako." Upesi, angalieni, huyo hapo Uzao uliokusudiwa Uzima wa Milele. "Wote alionipa Baba watakuja. Hakuna mtu awezaye kuja, Yeye asipoita." Mnaona? "Wote alionipa Baba," wakati uliopita, "watakuja."

28 Basi wakati Nuru hiyo ilipomulika kwenye ile Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani, upesi, si kama hao wasomi wenye elimu, wakisimama pale wakikosoa, walidhani walikuwa katika Kundi hilo, bali hawakuwa, walimwita Beelzebuli, lakini mara alipoifikia hiyo Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani, Nuru hiyo ilimulika juu Yake, akasema, "Bwana," ikawa Hai, mnaona, ikaihuisha, "Naona ya kuwa Wewe ni nabii. Tunajua Masihi, atakapokuja, atafanya kazi ya namna hii."

29 Akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye." Loo, jamani! Hilo lilitosha. Mnaona? Ati nini? "Wote alionipa Baba . . . " Tunapanda tu mbegu, Mungu huziweka mahali popote atakapo. Zingine huanguka kando ya njia; zingine zinatokea kwenye miiba kwa siku chache, nayo michongoma inaisonga na kadhalika, na zingine zinaenda mahali pafaapo. Sijui ziko wapi, tunazipanda tu.

30 Asanteni. Mungu awabariki. Sasa hebu na tulisome Neno. Sasa nataka kuchukua, kama ni sawa, nafasi usiku wa leo, kufundisha kwa namna fulani tu, sio kitu kisicho cha kawaida, mafundisho kidogo tu. Na labda Jumapili alasiri, Bwana akipenda, ningetaka kufundisha kanisa ujumbe mdogo, Bwana akiruhusu.

31 Ilikuwa vizuri sana kwa hawa ndugu hapa kuniambia, "Ndugu Branham kama ninii . . . " Barua nzuri na wote wakaitia sahihi. "Tunakuweka mimbarani, hubiri yaliyo moyoni mwako." Mimi . . . hiyo ni . . . nisingeweza kuwa na uhuru zaidi ya huo. Na kwa hiyo, ni—ninashukuru sana kwa ajili ya kundi la watu, wahudumu, wachungaji. Nami . . .

32 Mara nyingi wahudumu wanashuku kwa sababu (Wana haki ya kushuku.) wao ni wachungaji nao wanataka kujua kile kondoo wao wanakula, hiyo ni kweli. Wanapaswa kujua. Naye mtu aliye na hadhi na heshima asingeweza kumdhuru mtu yeyote ama kondoo yeyote, sikuzote angejaribu kumpa vitamini, hata hivyo, amweke kwe—kwenye kundi. Kwa hiyo labda Bwana atatupa vitamini kwa Maneno yale yale ambayo tumesikia mara nyingi.

33 Hebu na tufungue, usiku wa leo, kwenye Kitabu cha Pili cha Wafalme na kusoma tu sehemu ya Maandiko. [II Wafalme 1:1-8—Mh.]

> *Ikawa, baada ya kufa kwake Ahabu, Moabu wakawaasi Israeli.*
>
> *Naye Ahazia akaanguka chini kutoka baraza la chumba chake cha juu, huko Samaria, akaugua, akatuma wajumbe, akawaambia, Enendeni mkaulize kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni, kwamba nitapona ugonjwa huu.*
>
> *Lakini malaika wa* B*WANA* *akamwambia Eliya, Mtishbi, Ondoka, uende . . . ukakutane na hao wajumbe wa mfalme wa Samaria, ukawaambie, Je, ni kwa sababu hapana Mungu katika Israeli, hata mnakwenda kuuliza kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni?*
>
> *Sasa* basi, B*WANA* *asema hivi, Hutashuka katika kile kitanda ulichokipanda, bali hakika utakufa. Eliya akaondoka.*
>
> *Wale wajumbe waliporudi kwake, aliwaambia, Mbona sasa mmerudi?*
>
> *Wakamwambia, Mtu mmoja alitokea akaonana nasi,* akasema hivi, *Enendeni, rudini kwa mfalme, yule aliyewatuma, mkamwambie,* B*WANA* *asema hivi, Je, ni kwa sababu hapana Mungu katika Israeli, hata uwatume kuuliza kwa Baal-zebubu, mungu wa Ekroni? basi hutashuka kutoka katika kile kitanda ulichopanda, bali hakika utakufa.*
>
> *Akawaambia, Je, mtu yule aliyetokea, . . . akaonana* nanyi, *akawaambia* ninyi *maneno haya, alikuwa mtu wa namna gani?*
>
> *Nao wakamjibu, Alikuwa ni mtu mwenye malaika, . . .* amejifunga *mkanda wa ngozi kiunoni mwake. Naye akasema, Ndiye yule Eliya Mtishbi.*

34 Sasa, katika Yeremia kwa ajili ya somo, kama ningeliita, katika Yeremia mlango wa 8 na kifungu cha 22:

> *Je, hapana zeri katika Gileadi; huko hakuna tabibu huko? mbona basi haijarejea afya ya binti ya watu wangu?*

35 Nami ningetaka kuchukua somo, kama lingepaswa kuitwa hivyo, fungu, hasa, kama neno dogo la *Kwa nini*? K-w-a n-i-n-i. *Kwa Nini*?

36 Nami natumaini sipazi sauti sana huko nyuma, kama mhandisi wa hiki kwa namna fulani atakidhibiti. Wana nira ndogo shingoni mwangu usiku wa leo hapa, ambayo, kwa hiyo

na—natumaini sitapaza sauti sana. Na ni nzuri kwa sauti yangu yenye mkwaruzo.

37 Mungu anapowafanyia watu njia ya kuepukia, nao watu wanaikataa njia hiyo ya kuepukia, basi Mungu anauliza swali, "Kwa nini?" Nafikiri Yeye ana haki ya kuuliza. Kama Mungu akiwafanyia watu yote awezayo, nao watu wakatae kupokea msaada Wake, basi Yeye ana haki ya kuuliza ni kwa nini hawakufanya hivyo.

38 Ninaamini itakuwa hivyo kwenye Hukumu. Wakati Mungu amefanya kila maandalizi ambayo yangeweza kufanywa kwa ajili ya Kanisa na kwa ajili ya watu kisha wanayakataa, Mungu atatuuliza ni kwa nini hatukuyapokea, ninaamini hilo.

39 Sasa, tunaona ya kwamba huyu Ahazia alikuwa ni mwana wa Ahabu na Yezebeli, alikuwa ametoka kwenye familia iliyolaaniwa. Na unapoichukua familia inayowalea watoto wao katika mazingira mabaya, ni vigumu kutarajia kitu kingine chochote.

40 Sasa, Israeli ilikuwa taifa kitu kama taifa hili, ilifanya makosa yake yale yale ambayo taifa hili limefanya. Nasi tunaona ya kwamba Israeli walikuja kutoka Misri na kuwafukuza wenyeji kutoka nchini na kuimiliki nchi, vile vile tulivyokuja kutafuta oasisi, na kuwasukuma nyuma wenyeji huku na kuimiliki nchi. Israeli walipata kibali mbele za Mungu, tunaamini ya kwamba baba zetu wasafiri pia walikipata. Israeli katika hatua zake za mwanzoni ilitoa watu mashuhuri, vema, kwa mfano walikuwa na Daudi, Sulemani, Yoshua, watu mashuhuri, nasi tulikuwa na Washington, Lincoln, na . . . watu mashuhuri.

41 Lakini hatimaye, Israeli, katika siasa zake, ilijifanyia na kuweka haini kwenye kiti cha enzi, Ahabu, mwaminio nusu, mfuasi vuguvugu wa kanisa. Naye Ahabu hakuwa m—mkora kama alivyokuwa mke wake. Yeye ndiye ambaye angeweza tu kumwongoza Ahabu, kwa njia yoyote aliyotaka kumfanya apitie, alifanya hivyo.

42 Na si lazima uwe wa kiroho sana upate kuelewa ninachozungumzia. Ni ule mfumo ulio nyuma yake. Lakini katika siku hiyo walikuwa na nabii, nalo jina lake lilikuwa Eliya, naye alikuwa ni mcha Mungu asiye na woga.

43 Nami nafikiri wengi wenu ninyi Wanademokrasia vimbelembele mliouza haki zenu za mzaliwa wa kwanza kwa siasa, kufanya jambo ovu kama hilo mlilofanya, Mungu na awarehemu. Naam, bwana. Siku moja taifa hili lilijua kitu hicho cha kale, bali limekisahau. Lilijiuza, kwa sababu kanisa lilipata uvuguvugu na kumwacha Mungu. Hiyo ni kweli kabisa.

Afadhali niachane na hayo, maana nilisema sitahubiri juu ya jambo hili. Sasa, tunapoendelea, lakini mnajua ninachowazia.

44 Angalieni, lakini katika siku iyo hiyo Mungu alimtuma mtu mwenye nguvu nchini, kabla tu ya hapo kukaja tauni iliyoenea nchini kote, naye Mungu akathibitishwa.

45 Sasa, kwenye huu, baada ya kifo cha Ahabu, mwanawe alipachukua mahali pake, na, Hezekia, naye akatawala huko Samaria. Ndipo siku moja akitembea kwenye madirisha, alianguka kisha ugonjwa fulani ukaingia mahali alipoumia. Na sasa, badala ya kufuata, kama vile mababu walivyofanya, kumtaka Mungu shauri juu ya jambo hilo, yeye alituma watu kwa ile sanamu, Beel-zebubu.

46 Ni ajabu kwamba mtu anayedhaniwa kuwa ni Mwisraeli angekitaka shauri kitu kama hicho, badala ya kumrudia Mungu yeye yule aliyewaleta katika nchi hiyo na kuwapa. Kwa sababu alikuwa akijaribu kufuata mwelekeo wa siku hizo, na kumfuata baba na mama yake.

47 Hilo ndilo lililotendeka makanisani siku hizi, kupita kiasi. Tumeyaacha matumizi ya kiroho ya kanuni ambazo taifa hili linazitetea nalo limejiingiza kwenye siasa, na muungano, na burudani, na tumbo lililoshiba, na gari jipya, na makazi mapya, na—na kuziacha kanuni halisi za mambo, kanuni halisi za Ukristo.

48 Ni vibaya sana hatuna budi kusema mambo haya, lakini mtu fulani hana budi kuyasema, nayo hayana budi kutimia. Inatubidi kuwa wakweli, na waaminifu, na wanyofu. Wala huhitaji tafsiri ya kiroho, kwa sababu yako mbele ya macho yako, unaweza kuyaona.

49 Lakini sisi, kama walivyofanya katika siku hizo, tumeuza haki zetu za mzaliwa wa kwanza kwa mlo wa dengu, nasi tutavuna tu tulichopanda. Na umepita sasa, na uamsho tuliokuwa nao ukienea kote nchini, umekufa ukasalia mwali mdogo unaoungua polepole hapa na pale, ama chochote kile. Hatutaki kuliamini, bali ni kweli. Hiyo ni kweli.

50 Nasi tulitoka tukapanda lundo la mbegu kubwa za kimadhehebu, na wakati Roho aliposhuka, tulivuna nini? Zao la kimadhehebu. Kama tungalikuwa tumepanda Neno la Mungu, tungevuna Kanisa la Mungu, kama tungefanya hivyo, lakini tulienda upande mwingine.

51 Mvua huja juu ya nchi kuinywesha maji. Na kama ninii . . . Aina yoyote ya mbegu iliyo shambani, hiyo ndiyo inayokuza. Hiyo ni kweli. Na kwa hiyo Roho Mtakatifu yeye yule anayelikuza Kanisa la Mungu aliye hai hukuza magugu pia, ya *kimadhehebu*. Lakini mnaona kile tumevuna, "Milioni moja zaidi katika mwaka wa '44," kwa ajili ya Wabaptisti, na kadhalika na kuendelea. Na hayo ndiyo tumevuna, sawa kabisa na vile tulivyopanda. Daima itakuwa hivyo.

52 Nao Israeli walikuwa, walivuna tu walichokuwa wamepanda. Naye huyu kijana alikuwa amekuja sasa kuchukua

mamlaka. Na badala ya kutuma watu na kumtafuta Mungu, kwa watu waliokuwa wamekuja kule kwenye uchumi huu mkuu ambao Mungu alikuwa amewapa, alituma watu huko kwa, ile sanamu maarufu ya siku hizo, Beelzebuli, dini iliyopendwa sana miongoni mwa watu; ni wachache tu waliokuwa wameshika Mwenge.

53 Naye Eliya alikuwa ndiye nabii mkuu wa siku hizo. Naye alikuwa amesahau habari za Eliya, hakumjali Eliya, kwa sababu Eliya angalimwambia mahali alipokuwa amesimama. Kwa hiyo, hawataki kujua ukweli ni upi, afadhali wachukue njia hii nyingine, bila kutambua ya kwamba utavuna unachopanda, hasa. Hiyo ni kanuni ya maumbile, unafanya hivyo; ni kanuni ya Roho, bila shaka inakubidi kufanya hivyo.

54 Sasa, lakini mnajua, Mungu hufunua siri Zake kwa manabii Wake. Biblia ilisema, katika Amosi, "Hakika Mungu hatafanya neno, bila kuwafunulia manabii Wake."

55 Ndipo basi wakati wajumbe hawa wakienda zao kukutana na kuhani, na kujua kutoka kwa Beelzebuli hali ya mfalme wao, na kile kingekuwa matokeo yake, hawakutaka kuchukua njia ya Mungu kujiweka sawa na Neno la Mungu, kufuata njia ya Mungu ya kufanya mambo, walitaka kuishi vyovyote walivyotaka na bado wawe wa kidini.

56 Na hilo ndilo, taifa hili limefikia siku hizi. Kamwe halitaki kujiweka sawa na Mungu, linataka kuishi vyovyote litakavyo, bali linataka kuwa la kidini, kwa hiyo litachukua njia iliyo rahisi sana ya kutokea, daima linapata hiyo. Maji hupenya kiwango chake, daima. Sasa, walikuwa na mkono mwingine wa kuegemea, hawakumhitaji Yehova tena. Hawakutaka njia hiyo kali, walitaka kuishi kwa tamaa zao wenyewe na mitindo yao wenyewe, na hata hivyo wangeweza kuwa wa kidini.

57 Lakini kumbukeni, huko chini kabisa kwenye lile pango, alirudi nyuma mzee mwenye nywele nyingi, kitu kilichoonekana kama mdudu mwenye manyoya huko nyuma, lakini chini ya maskini ngozi hiyo ya kahawia na mikono iliyokonda, ulipiga moyo ambao Mungu aliishi ndani yake.

58 Akasema, "Eliya, simama uende kule ukakutane nao." Loo, jamani! Tunachohitaji leo hii ni Eliya mwingine, asiyeogopa kusema Kweli. Akapanda kule na kusimama njiani, amejifunga kipande cha ngozi ya kondoo, ama ngozi, kiunoni mwake *hapa* cha kujifunga, naye huyo hapo amesimama, uso wake umejaa manywele.

59 Na—nami nadhani hakuoga kila usiku, na kutumia uma na visu vyake jinsi tunavyofanya hapa Hollywood, na kuangaza jinsi tufanyavyo, lakini hata hivyo, Mungu alikuwa pamoja naye, Mungu alikuwa ndani yake. Tunasisitiza sana mapokeo ya siku hizi.

60 Sasa, tunaona, sasa, alisimama njiani wakati hawa wajumbe walipokuja, naye akasema, "'Ni kwa sababu…' Nenda ukamwambie, 'Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Hivi hakuna nabii hapa? Hiyo ndiyo sababu?'" Loo, kulikuwako na Mungu, na kulikuwako na nabii! Lakini ilikuwa ni ukaidi wa huyo mfalme mwenyewe, hakutaka kujiweka sawa na Mungu na nabii Wake. Na hiyo ilikuwa ndiyo sababu mfalme alikuwa akitafuta njia iliyo rahisi kuliko zote kutoka kwa mambo haya. Akasema, "Je, ni kwa sababu hakuna nabii, hakuna Mungu katika Israeli? Hakuna mwingine, hakuna njia ya kupata kujua?"

61 Nashangaa, siku hizi, kama ni leo tunatafuta faraja. Tumepoteza tu…tumeacha likizo kadhaa. Watu wanatoka na kwenda kulewa kwenye sikukuu hizo, wao ni walimu wa shule ya Jumapili, wafuasi wa kanisa, wanakwaya, wanatoka wanaenda kunywa pombe na kufanya karamu, wanacheza kamari, na—nao watu wanaishi tu watakavyo, na hata hivyo wao ni wafuasi wa makanisa ya juu sana yaliyoko mjini, baadhi ya hadhi za juu sana za mfumo huu wa kikanisa la kiakili, ambao unaitawala nchi hii, ulioko.

62 Na kushangaa, "Kwa nini? Kwa nini hawaji?" Wanatafuta anasa, wanatafuta amani, wanabadilisha, ibilisi anabadilisha vitu kama hivyo vyenye vurugu kupachukua mahali pa tukio zuri sana lililojazwa na Roho, ambapo furaha ya Bwana inaweza kuja juu yao na kuwapa amani na raha.

63 Wanapenda anasa za ulimwengu kuliko wanavyoupenda Ufalme wa Mungu, maisha yao yanathibitisha hilo. Hiyo ni kweli kabisa. Kile wanachoishi kinaonyesha. Hakuna tofauti ndani yao, inaonekana kuwa, ni nani mwaminio na ni nani asiye mwaminio, ukizungumza nao, wanafanya tu mizaha michafu vivyo hivyo, nao wana mashirika yao na kadhalika, na kuendelea tu kama walimwengu wengine.

64 Niliishi ng'ambo ya barabara kutoka pa—parokia mashuhuri ya hadhi kubwa ya Wakristo, kama wanavyojiita, na kila Jumamosi usiku kwenye sakafu ya nyumba ya mchungaji, mbona, kamwe hujawahi kusikia makelele kama hayo, na twisti, na roki, na bugi-bugi, na upuuzi huo wote mwovu, na kupiga mayowe! Halafu Jumapili asubuhi wanaenda kanisani wakiwa na sura ya uchaji.

65 Ndugu, wakati Roho Mtakatifu anapoingia katika maisha, Yeye hubadilisha maisha hayo kutoka chini ya miguu yake hadi juu ya kichwa chake. Na sehemu ya kuhuzunisha, inanyemelea katika madhehebu yetu ya Kipentekoste. Inaingia mle kwa sababu, kama tu vile imekuwa daima…

66 Wakati Israeli walipoona hayo mataifa mengine yalikuwa na mfalme, basi walitaka kutenda kama mataifa mengine. Maskini nabii huyo aliwajia, Samweli, naye akasema, "Hamna budi

ku-. . .ninyi ni watu tofauti, hampaswi kuwa kama wao, Mungu ndiye Mfalme wenu." Akasema, "Hivi nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana, ila lililotimia? Hivi nimewahi kuwaomba pesa zenu, ama kuchukua fedha zenu, na kadhalika, kujenga majumba makubwa ya heshima na chochote kile?"

67 Iliwabidi kusema kwamba hakufanya hivyo. Akasema, "Basi nisikilizeni." Naye alikuwa na Neno la Bwana. Lakini ilibidi hao watu wakubali ya kwamba kila kitu alichokuwa amesema kilikuwa ni Neno la Bwana, na kilikuwa kimetimia jinsi tu alivyosema kingetimia, lakini hata hivyo watu walitaka kufanana na watu wengine.

Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, kwamba makanisa yanajaribu kujifananisha na makanisa mengine, Kristo ndiye Mfano wetu. Hivyo hasa.

68 Sasa, hawakuutaka, hawakuutaka Ujumbe. Vipi kama mfalme huyo angejinyenyekeza? Vipi kama angalishuka kwenye. . .angeaibishwa, na kumrudia Mungu na kutubu? Ninaamini huyo mtu angaliishi, ninaamini Eliya angemjia na Neno la Bwana, naye huyo mtu angaliishi, lakini akaufanya moyo wake mgumu wala hakumsikia Bwana.

69 Naye Eliya akasema, "Enendeni mkamwulize, 'Je, ni kwa sababu hakuna—hakuna Mungu katika Israeli? Yeye hana nabii?'" La, alikuwa na nabii. Alikuwa na. . .Kulikuwako na Mungu, bali mfalme hakumtaka, na hivyo ndivyo ilivyo leo hii.

70 Ni kama tu m—mgonjwa anayeketi kwenye mlango wa daktari, akafa ameketi mlangoni, kwa sababu yeye ni mkaidi sana asiweze kuingia kunywa dawa aliyo nayo daktari kwa ajili yake. Kweli kabisa, kufa kwenye vipandio vya daktari, akiketi huko nje, naye daktari anasema, "Ninayo tiba ya ugonjwa wako," lakini yeye ni mkaidi sana kuingia na kuinywa.

71 Hilo ni jambo hatari, ja—jamaa angeweza kufa, naye angekufa, ameketi pale, wakati kuna dawa nyingi, wana sumu kwa ajili yake lakini wao. . .hatainywa, yeye ni mkaidi sana. Vema basi, huwezi kumlaumu daktari, wala huwezi kuilaumu hiyo dawa, ni huyo mtu, yeye ndiye.

72 Ndivyo ilivyo siku hizi, wanaume na wanawake wataketi kanisani, kwenye benchi la kanisa, na kuisikia Injili isiyoghoshiwa, na nguvu za Roho Mtakatifu, na kuona madhihirisho na ushahidi wa Roho Wake, wa Kristo aliye hai, aliyefufuka, kisha wafe katika dhambi, wameketi kwenye benchi la kanisa. Si kwa sababu hakuna zeri, si kwa sababu hakuna tabibu, lakini ni kwa sababu watu ni wakaidi sana hawatakunywa dawa, wakijaribu kutafuta njia iliyo ndogo zaidi ya upinzani, wakipitia njia ya ulimwengu, wakiangamia katika uasi wa Kora.

73 Mnajua kile Kora alichofanya. Daima viongozi ndio wanaowavuruga watu, na kwamba waliangamia katika uasi wa Kora, hakika.

74 Usimlaumu daktari, usiilaumu dawa, lawama ni yako. Kama daktari anayo tiba, naye anayo kwa wingi, anakualika uje nawe hutakuja, basi si kosa la daktari, wala si kosa la dawa, ni kosa lako, kwa sababu hutakunywa hiyo dawa. Hiyo ni kweli.

75 Nao watu wanaketi makanisani, wanakufa kwenye benchi bila kumjua Mungu, bila kumpokea Roho Mtakatifu, kwa sababu wanafikiri itawabidi kuacha baadhi ya mambo ya ulimwengu. Afadhali wawe wafuasi wa kanisa ambalo lina jina kubwa zaidi, ama wanayowazia, heshima nyingi zaidi.

76 Je, umewahi kutambua njia ya Mungu ni kwamba, wachache huipitia njia hiyo? Nao wanadharauliwa na kukataliwa kwa sababu wao si wa ulimwengu, wao ni wa Mungu, watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme, wakitoa dhabihu za kiroho, hizo ni matunda ya midomo inayomsifu Mungu. Amina.

77 Dawa za daktari, mwajua kulikuwa na wakati ambapo hawakuwa na sumu yoyote kwa magonjwa kama vile ndui, maelfu walikufa kila mwaka kwa ugonjwa wa ndui. Hawakuwa na sumu ya dondakoo, ndipo maelfu wakafa kila mwaka wakiwa na sumu, au, bila kuwa na sumu yoyote walikufa kwa dondakoo. Lakini sasa wana hiyo sumu, wana chanjo ya vitu hivyo.

78 Naye daktari hupataje dawa hizi kwa vyovyote vile? Kitu gani, wanalifanya—wanalifanya kwa njia gani? Mnajua wanavyofanya? Wanaweka vitu vingi pamoja, sumu kidogo, kisha kiuasumu kidogo, wanavichanganya pamoja mpaka watakapochanganya fomula fulani. Ndipo wanachukua—wanachukua nungubandia, nao wanamdunga nungubandia dawa hii, kama atapona hiyo, basi wanakupa wewe. Halafu basi . . . na kama ni . . .

79 Mnaona, ni kuua ugonjwa ulio mwilini mwako, *kiasi fulani* cha sumu, *kiasi fulani* cha kuitibua sumu hiyo. Sumu nyingi kupita kiasi ingekuua, kiua sumu kingi kupita kiasi hakingekufaa kitu, dawa isingefaa, haina budi kuwa ni fomula yenye uwiano.

80 Na baadhi ya dawa kutoka kwa daktari, anaweza kuzitoa, kwa mfano, kama penisilini, moja ya uvumbuzi mkuu ambao . . . Wao wanafikiri ni uvumbuzi. Vema, nilipokuwa Afrika Kusini nilimwona mwenyeji kule, na wakati yeye angeninii . . . wakipata kidonda mguuni mwao, ama *kitu kingine*, hicho kidonda kinazeeka, wanatafuta chungwa la kale, limewekwa chini ya mti mahali fulani, ambalo limeota kuvu, nao wanasugulia hilo chungwa humo ndani, wamekuwa wakifanya hivyo kwa mamia na mamia ya miaka, nao wanapata afya. Ni kitu gani? Penisilini, hakika.

81 Kwa hiyo wanafikiri wao ni werevu, Mhotentoti huko Afrika alijua hilo miaka elfu moja iliyopita. Mungu tayari amemwambia jinsi ya kujishughulikia mwenyewe, halafu tunafikiri ya kwamba ni kitu cha akili tulicho nacho. Sasa, penisilini, wakati mwingine kuzidisha kiasi kutamwua mgonjwa na baadhi yao inawasaidia, kuna swali hapo.

82 Wanadai ya kwamba siku hizi, bila shaka, mwuaji namba moja, wanasema, ni ugonjwa wa moyo. La, ninatofautiana na hilo, mwuaji namba moja si ugonjwa wa moyo, mwuaji namba moja ni tatizo la dhambi, huyo ndiye mwuaji, jambo ndilo hilo. Ni dhambi, hiyo ndiyo mwuaji, sio ugonjwa wa moyo.

83 Watu wengi sana husema, "Sina budi tu kutenda dhambi. Inanibidi tu kuvuta sigara." Wanawake wanasema, "Sina budi tu kukata nywele zangu. Si—si—siwezi kupata nguo zingine zozote, inanibidi tu kuvaa walizo nazo." Mnajua shida ni nini? Wanatoa udhuru, hawajaijaribu sumu ya Mungu bado. Kama kamwe wakipata hiyo, wangechanjwa kutokana na upuuzi kama huo. Hiyo ni kweli. (Samahani.) Naam, ni kwa sababu hawajaijaribu sumu ya Mungu, wanakataa kuinywa.

84 Kwa kuwa wakati Roho wa Mungu anapokuwa ndani yako, Yeye hujilainisha na Neno la Mungu, na kama akilikana Neno la Mungu basi siye, hujadungwa sindano sahihi bado, hivyo tu. Hujachanjwa, dhambi ingali iko mlangoni, kutokuamini Neno. Kwa hiyo inahitaji sumu ya Mungu kuua dhambi, nayo dhambi ndiyo mwuaji namba moja. Naam, ndivyo ilivyo. Inaua, na inaua kabisa. Kwa hiyo tunajua ya kwamba ni—kwamba ni ninii . . . dhambi ndiyo inayoua. Kwa hiyo ni sumu, watu wanakataa tu kuinywa, hawaipendi, hawapendi wazo la kuzaliwa upya.

85 Sasa, tunajua ya kwamba kuzaliwa kwokwote ni mchafuko, sijali kama kuko kwenye zizi la nguruwe ama kama kuko kwenye chumba cha hospitalini kilichopambwa kwa rangi ya waridi. Kuzaliwa kwokwote ni mchafuko, na kuzaliwa upya si kitu pungufu, ni mchafuko. Hiyo ni kweli. Kutakufanya upige nduru, na kulia, na kufanya yasiyofaa, kana kwamba ulikuwa katika mchafuko mbaya sana uliopata kuwa ndani yake, lakini kutakufaa.

86 Yesu alisema, "Chembe ya ngano isipoanguka ardhini ikafa, inakaa peke yake." Wala watu hawataki kufa, unataka kuwa hai ulimwenguni, na bado unataka kuwa wa kidini, kwa hiyo unakubali wazo la kiakili juu yake. Halafu basi, unapofanya hivyo, ungali umekufa katika dhambi na makosa. Na hilo ndilo linalowafanya watu watende na kufanya jinsi wanavyofanya, kwa sababu roho iliyo ndani yao inatawala maisha yao.

87 Unasema, "Vema, watu wengine hufanya *hivi*." Vema, wewe si kama hao watu wengine, umekufa, na uhai wako umefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo na kutiwa muhuri kwa Roho

Mtakatifu. Unaona, hukuijaribu ile sumu; ni kwa sababu tu watu hawataki kuijaribu.

88 Sasa, huna budi kufa, huna budi kuoza. Hiyo ndiyo shida ya watu, badala ya kulilia madhabahuni: wanapata namna fulani ya mhemuko, wanaruka juu na kupeana mikono na mhubiri, wanatoka wanaenda na kuchukua namna fulani ya fundisho la sharti ama kanuni ya imani na kuikariri, na kusema, "Mimi ni mfuasi wa *Ninii*. Mimi ni mfuasi wa *Ninii*."

"Je, wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni *Nanii*."

89 Mkristo anapaswa kuwa kama Kristo, kuwa kama Kristo ni kuamini Neno. Na kama huliamini Neno, basi huwezi kuwa kama Kristo. Unawezaje kusema wewe ni Mkristo kisha ukane nusu ya Neno? Kama Roho Mtakatifu aliliandika Neno, Roho Mtakatifu hulithibitisha hilo Neno, na Roho Mtakatifu ni Neno. Neno likikaa ndani yako huleta ahadi za Mungu kwa kila mwaminio. Amina. Neno hilo linamaanisha "na iwe hivyo." Ninaamini kwa moyo wangu wote, ni Neno la Mungu aliye hai. Amina.

90 Angalieni, naam, kuzaliwa upya, hawataki kufa. Sasa, waliweka kitu fulani badala ya kuzaliwa upya. Kama... ibilisi...kama hutalichukua Neno la Mungu, basi ibilisi atakupa neno lake. Na hapo ndipo jamii ya kwanza ya mwanada-...ambapo jamii ya binadamu iliangukia kwa mara ya kwanza, ilikuwa ni kutokuliamini Neno la Mungu.

91 Njia bora zaidi ambayo Mungu angeweza kuliimarisha jeshi Lake ilikuwa ni kuwaimarisha kwa kilicho bora zaidi. Kama taifa letu...Tuna majasusi huko Uingereza, Uingereza ina majasusi hapa, ingawaje sisi ni marafiki. Tuna majasusi kote ulimwenguni, na ulimwengu una majasusi humu ndani. Wanaangalia, waone ni aina gani ya kombora jipya, ni kitu gani kipya, kisha wanarudi kwenye taifa lao, wanatafuta kitu cha kukabiliana na hicho. Kwa nini? Nao wanawavalisha watu wao, wanatayarisha mambo kwa ajili ya vita vya namna hiyo. Daima vinaendelea. Kuna vita kati ya ibilisi na Mungu, daima imekuwako.

92 Na kila mwaka wanapata kitu kipya. Zile ndege za kale walizotumia huko nyuma, zile P-38 za kale, na chochote zilichokuwa, waliziondolea mbali, wanazo jeti sasa. Springfield ya kale haifai kitu, wana bunduki ya kombora sasa. Maskini lile kombora angamizi limepitwa na wakati sana. Vema, hata zile treni za kale, injini za kale za mvuke, zilizokuwa zikivuta vitu hivyo huku na huko kwenye reli, zimepitwa na wakati. Hakika, wamepata kitu kipya. Daima wanafanya utafiti, kitu kipya, kitu kipya. Sasa, wanajaribu kuchimba chini ardhini, kutafuta njia ya kulikwepa bomu la atomiki, kitu kipya, kitu kipya.

93 Mungu alitoa kilicho bora kuliko vyote, hapo mwanzo, kwa ajili ya jeshi Lake kuu, lenye nguvu, na kamwe hajalazimika kukibadilisha, kwa sababu, kama nilivyosema jana usiku, uamuzi Wake wa kwanza ndio bora zaidi na wa pekee, Yeye aliwapa watu Wake Neno Lake.

94 Naye Shetani akahojiana nao, hoja dhidi ya Neno la Mungu, hivyo ndivyo ibilisi anavyofanya siku hizi. Yeye hujaribu kulihoji, akisema, "Sasa, hii ni *dhadhiri* tu kwamba haikubidi kufanya *hivi*. Ni *dhahiri* tu, tuna madaktari wazuri, hatuhitaji uponyaji wa Kiungu. Ni *dhahiri* tu, tuna washiriki wengi sana, hatuhitaji—hatuhitaji Roho Mtakatifu, hakuna Roho Mtakatifu."

95 Wanalihoji, wakijaribu kusema hao watu wamechanganyikiwa kiakili, wana mhemuko, kwa sababu, wao wenyewe, wamekufa katika dhambi na makosa wala hawajui lolote kuhusu nguvu za Mungu.

96 Inanikumbusha juu ya kafiri mmoja wakati mmoja alikuwa akishikilia, akihojiana, naye akasema, "Hakuna kitu kama Mungu."

Maskini mvulana mmoja wa mashambani, aliyevaa ja—jaketi la ovaroli, nywele zake zikining'inia usoni mwake, akapanda hapo, akaanza kumenya tofaa.

Yule kafiri akasema, "Mpumbavu, kwani unataka nini?"

Akasema, "Ninataka kukuuliza swali."

Kasema, "Vema, ni kitu gani?"

Akatoa kokwa la hilo tofaa, akaliuma, akaanza kula, kasema, "Je, hilo tofaa ni chungu ama tamu?"

Ndipo huyo kafiri akasema, "Sijui kwa sababu silili."

Akasema, "Hivyo tu ndivyo nilivyokuwa nikiwazia." Ja—jambo ndilo hilo. Nao watu wakamcheka huyo kafiri akaondoka jukwaani.

97 Kwa nini? Kwa sababu hakuwa amewahi kulionja, hakuwa amewahi kulijaribu, hakuwa amewahi kunywa hiyo sumu, haleluya, ya nguvu za Mungu kukuchanja kutokana na kutokuamini kwokwote kwa Neno la Mungu.

98 Roho Mtakatifu halisi ataitikia kila sentensi kwa "Amina." Hatasema, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama *hiki,* hakuna kitu kama *hicho*. Vema, *hoja* tu, kasema hatupaswi kulifanya *hivi*, hatupaswi kulifanya *vile*."

99 Kile Mungu asemacho, Roho Mtakatifu alisema, "Amina." Kila sentensi, kila Neno, kila kifungu katika Biblia kinaitikiwa kwa "Amina." Naam, bwana.

100 Kuzaliwa upya kunaleta mchafuko, bali huleta Uzima mpya pamoja nako. Hiyo ni kweli. Mmea, chochote kile, mbegu haina budi kuoza ili kuleta uhai mpya kutoka kwake. Mwenye dhambi

hana budi kufa na kuoza kwa mawazo yake mwenyewe. Maisha yake mwenyewe hayana budi kuoza ili kwamba Uhai mpya uweze kukua kutoka kwake; ni mchafuko, bali ni mchafuko wenye utukufu, huleta Uzima mpya.

101 Hilo ndilo kanisa linalohitaji siku hizi, bali wanalikwepa kwa mafundisho ya sharti na kadhalika, kujaribu kukwepa mawazo ya kufa kwa nafsi zao, wanataka kuishi kwa nafsi zao. Yeye aishiye kwa nafsi yake, anaishi kwa ajili ya... yeye mwenyewe na ibilisi, yeye anayejikana mwenyewe atapata maisha yake katika Kristo naye atakuwa kiumbe kipya.

102 Sasa, tunaona jinsi wanavyopata sumu hizi. Wanazichukua, kama nilivyokuwa nikisema, nao wanachanganya fomula fulani, *sayansi* hufanya hivyo, na kumpa nungubandia. Sasa, kila mtu hana asili kama ya nungubandia, kwa hiyo itawaua wengine, itawasaidia wengine, tunajua hilo.

103 Lakini, mnajua wakati kulikuwa na wakati ambapo Mungu hakuwa na sumu nzuri sana, sumu Yake ilitokana na kondoo na mbuzi. Lakini wakati mmoja Mungu alikuwa akitaka kuikamilisha sumu Yake, kwa hiyo Yeye kamwe hakujaribu kumpa nungubandia, alijipa Mwenyewe. Alikunywa hiyo sumu Mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu Kristo, aliyetiwa Mafuta, Mungu alifanyika mwili kusudi adungwe hiyo sumu katika mwili Wake Mwenyewe.

104 Daktari yeyote mzuri ataijaribu sumu mwilini mwake mwenyewe, wakati hakuna mtu mwingine atakayeijaribu. Wala hapakuwapo na mtu mwingine ambaye angeweza kufanya hivyo ila Mungu. Kwa hiyo akashuka, Yehova, naye akafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu na kudungwa sumu hiyo Mwenyewe.

105 Kwenye Yordani wakati alipokuwa amesimama pale, Yohana alishuhudia, kasema, "Nilimwona Roho wa Mungu kama hua, akishuka juu Yake." Ndipo akapokea hiyo sumu na hiyo chanjo kutokana na dhambi na mauti. Alizaliwa na mwanamke, naye akaipokea hiyo sumu, nao wakamwangalia waone kitakachotukia. Nao wakamwona katika kesi Yake, wakamwona wakati alipokuja mbele ya mabishano, daima alishikilia Neno la Baba. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

106 "...?...mnajua hakika Mungu asingefanya jambo kama hilo," alihojiana hilo na Hawa, lakini wakati alipokuja dhidi ya Kristo, aligonga huo Waya wa volti laki moja, manyoya yalivurugika alipokuja na hoja zake, kwa sababu Yeye alikabiliana naye moja kwa moja kwa BWANA ASEMA HIVI.

Kasema, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu Nawe una njaa, kwa nini usigeuze mawe haya yawe mkate na ule?" Kutoa hoja. "Ungeweza kufanya hivyo."

Hakika angeweza, bali alirudi tena, “Imeandikwa, ‘Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno, litokalo katika kinywa cha Mungu.’”

107 Walimwangalia, wakaona hiyo sumu ilishikilia kwa kila hali. Wakati ulipowadia, akikabiliwa na mauti, ile sumu ilishikilia. Walipomtemea mate usoni Mwake, wakamdhihaki, ile sumu ilishikilia.

108 Hapo ndipo mahali pa kuamini uwe na sumu usiwe nayo, hilo hapo jaribio lako. Mtu fulani aseme jambo fulani kukuhusu na kusema, “Wewe ni maskini mtakatifu anayejibingirisha . . . ” Vema, unaacha kwenda kanisani, halafu useme umechanjwa, useme umepokea sumu, ile zeri.

109 “Je, hapana zeri katika Gileadi; hivi hakuna tabibu huko? Kama ipo, basi kwa nini binti . . . ?” Kumbukeni, si mama, Yeye alimtaliki, lakini huyo binti ndiye Kanisa *hili*, unabii huo unalihusu *hili*. “Kwa nini binti ya watu Wangu, afya yake haijarejea basi?”

110 Huyu hapa akiwa na upungufu wa damu usiku wa leo, hiyo ni kweli, nusu *huku* na nusu *kule*, na wote wamevurugika, na kila namna ya taratibu na chochote kile, na kutengwa katika udugu, wametawanyika kila mahali, nusu wakiamini *hili*, na nusu wakiamini kanuni za imani, na nusu wakiamini madhehebu, nusu wakiamini *hili* na *lile*. Vema, jamani, afya yake inapaswa kuwa imesimama kikamilifu, yenye mashavu mekundu, pamoja na Neno la Mungu na nguvu za kufufuka Kwake!

111 “Kwani binti ya watu Wangu ana shida gani basi? Yuko wapi binti Yangu? Ninatuma ishara Zangu miongoni mwao namna hiyo, nao wanasimama tu na kutoka nje. Binti ya watu Wangu ana shida gani?” wakati limeelezewa na kuthibitishwa kwa Neno. Nayo Biblia ilisema kama ninii . . . daima kuliamini Neno. Neno limethibitishwa, basi huwezi kutokuliamini, bali unahoji, ukimruhusu Shetani akuambie niani mwako.

112 Jana usiku ulipoinua mkono wako ya kwamba ulikuwa mwenye dhambi, wala hukutaka kufa mwenye dhambi, nami nikakuita jukwaani, ukageuka na kutoka nje. Kuna shida gani? Ulimwacha Shetani atoe hoja, “Utapoteza kazi yako.” Afadhali nipoteze kazi yangu kuliko kupoteza Maisha yangu. “Mke wako atakuacha.” Afadhali nipoteze mke kuliko kumpoteza Kristo wangu. “Mumeo ama jirani ya—yako atakudhihaki.” Afadhali jirani yangu anidhihaki na niwe sawa na Mungu.

113 Lakini, unaona, unasikiliza hoja, ndivyo hivyo, unaninii tu . . . umekuwa na mambo mengi sana ya bandia. Hivi hutambui, ewe rafiki, ya kwamba kila wakati kitu cha bandia, hutangaza kwamba kuna kilicho halisi? Hakika, hutangaza.

114 Angalia, Mungu alijidunga Mwenyewe sumu Yake, wakaangalia. Katika wakati ambapo waliweka kitambaa juu ya uso Wake, Yeye angeninii . . . angeweza kuyatambua

mawazo katika mioyo ya hao watu, nao wakaweka kitambaa usoni Mwake, na kumpiga kichwani kwa fimbo, na kusema, “Sasa, kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga, nasi tutakuamini,” lakini ile sumu ilishikilia. Amina. Hakuwa akifanya vitimbi.

115 Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu siku hizi, wanataka kuigiza kidogo. Hiyo ndiyo shida ya Pwani hii ya Magharibi, mna Hollywood nyingi kupita kiasi ndani yake, mna mng’ao mwingi kupita kiasi. Roho Mtakatifu hang’ai, Roho Mtakatifu humeka. Kuna tofauti kati ya kumeka na kung’aa. Kanisa hung’aa kwa mpango wake mkubwa, lakini Roho Mtakatifu humeka katika unyenyekevu, unyenyekevu, kupatana na Neno, kuliamini Neno.

116 Maskini yule mtakatifu wakati mmoja, akiketi kanisani . . . Majuma machache yaliyopita nilipaswa kuwa katika mkutano wa Chicago, ndipo mhudumu mashuhuri kule akasema, “Hatuwezi kuwa na Ndugu Branham kwa sababu ya fundisho lake.” Nami sihubiri Fundisho lolote miongoni mwao, bali alitaka tu kusema hivyo.

117 Naye akamchukua jamaa fulani mkubwa mno kutoka kwenye taasisi fulani kubwa kule. Naye akaja akitembea, kifua chake, akiwa na makaratasi ya kutosha yaliyowekwa pale ilionekana kana kwamba angeweza kufanya chochote nayo, akatembea kifua mbele, akakitupa hicho nyuma, kitabu hiki kikubwa, katika mazungumzo ya kielimu. Jamani, yalikuwa ni ya ajabu, mazungumzo yake ya kielimu, bali hapakuwa na Roho ndani yake!

118 Baada ya kitambo kidogo akaona hilo halikuendana na watu wa Mungu, kama tu vile Sauli akijaribu kumvisha Daudi vazi lake la kikanisa, mtu wa Mungu, halikumwenea. Wala ujumbe wa kiakili hauendani na Kanisa lililojazwa na Roho, hawana budi kuwa na nguvu za Roho Mtakatifu na dhihirisho. Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao,” hawana budi kuwa nazo.

119 Ndipo mtu huyo akagundua kwamba halikuchukuana na Wapentekoste, akakunja vitabu vyake na kushuka chini huku ameinamisha kichwa chake. Maskini mtakatifu mmoja aliyekuwa ameketi pale pembeni akaja akaniambia baadaye, kasema, “Kama angalipanda jinsi alivyoshuka, angalishuka jinsi alivyopanda.” Kwa hiyo hivyo ndivyo karibu ilivyo siku hizi.

120 Tunachohitaji ni, kumrudia Roho Mtakatifu, kurudi kwenye Biblia, kurudi kwenye nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo, na si hoja hizi zote hapa, na usomi, na kadhalika, bila shaka.

121 Walikuta kwamba ilishikilia, ilishikilia katika saa ya kufa, ilishikilia katika saa ya Gethsemane, ilishikilia katika mambo hayo yote, ndipo Yeye akafa. Alikufa, kama nilivyosema jana usiku, mpaka kila kitu, kikatangaza ya kwamba amekufa.

Mwezi, jua, na nyota, nchi, matetemeko ya nchi, kila kitu kilithibitisha alikuwa amekufa; jua likatua mchana.

Yule askari wa Kirumi akasema, “Kwa kweli huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu.”

Yudasi akasema, “Niliisaliti Damu isiyo na hatia.”

Pilato akasema, “Nipe maji, hebu nikanawe mikono yangu. Sitakuwa na uhusiano mwingine nayo.”

122 Alikufa, Naye akaenda pamoja na chanjo hiyo, bali ilikuwa ni chanjo ya Uzima wa Milele, katika siku ya tatu ingali ilishikilia. Baada ya unabii wa Mungu kutimizwa, Yeye alifufuka katika siku ya tatu akiwa hai, Kanisa liliona jambo hilo na kushangilia.

“Sasa,” Yeye akasema, “hamna budi kuchanjwa pia, bali ninawatakeni mwende *huko* juu na kungoja mpaka mtakapopata chanjo yenu.”

123 Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, hawakupanda na kungojea chanjo yao. Walienda kwenye seminari na kupata B.A. yao badala ya kwenda kuchanjwa, wapande waende wakachanjwe Zeri ya Gileadi katika mishipa ya nafsi yao. Hiyo ni kweli.

124 Walipanda kule kwenye Siku ya Pentekoste, wote walikuwa wamekusanyika pamoja. Waliamini alikuwa amefufuka katika wafu, walikuwa wamezungumza Naye, Naye aliahidi angeshusha chanjo hiyo yote. Basi wote walipokuwa wamekusanyika pamoja, ile Zeri ikaanza kuwashukia, nazo Ndimi zilizogawanyika zikakaa juu yao kama moto. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na kukimbia huko nje, wakaanza kunena kwa lugha zingine kama Roho alivyowajalia kutamka.

125 Kulikuwako na mtu ambaye, siku chache hapo kabla, alikuwa amemkana Yesu, akasimama juu ya sanduku la sabuni, ama kisiki, na kusema, “Enyi watu wa Uyahudi, na kwenu mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu: Watu hawa hawajalewa, kama mnavyodhania, kwa kuwa ni saa tatu ya mchana. Lakini hii ni ile chanjo iliyokuwa ije, kwamba angechanja kutoka kwa dhambi, kutoka kwa maradhi, kutoka kwa mauti, kutoka kaburini, kuingia Uzima wa Milele.”

Waliona ilikuwa imetenda kazi kwa Yesu wakati walipochomwa mioyo yao, nao wakawaambia, “Waume na ndugu, tufanye nini?”

126 Sasa, walikuwa na daktari pale, jina lake lilikuwa ni Dk. Simoni Petro. Walikuwa na tabibu, nao walikuwa na chanjo nyingi, ikithibitisha, wote walikuwa wamelewa hiyo. Kweli waliipokea kwa njia kubwa.

127 Nao walikuwa na Dk. Simoni Petro pale, akasema, “Sasa, hebu kidogo, mkitaka kujua jinsi ya kuchanjwa, nitawapa maagizo. Wala msijipumbaze nayo, iwekeni tu, kwa sababu

itakuwa ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.

128 "Nitawapa maagizo ya Milele kwa ajili ya chanjo hiyo. Mkitaka kuipokea Zeri hii, Zeri hii ya Gileadi, chanjo hii kutoka kwa dhambi na mauti, pokeeni maagizo haya." Daktari yeyote mzuri anayepima dawa yake, huipima ipasavyo. Nitakwambia, ndugu, aliwaambia basi, akasema . . .

129 Sasa, siku hizi wameweka vitu badala ya hayo maagizo, wanajaribu kusema, "Peana mikono. Nyunyizia kidogo," ama kitu kama hicho, lakini Petro alisema, "Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtachanjwa. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Bila shaka.

130 Kama daktari akiandika maagizo . . . Kuna shida gani leo? Kama daktari huyo akiandika maagizo kwa ajili ya ugonjwa huo, hayo yalikuwa yawe ni ya Milele . . . Umbali gani? "Kwa watoto wenu." Wanasema iliishia kwa mitume, haikuisha. Daktari, Simoni Petro, alisema, "Ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Hii ni chanjo yao.

131 Kuna shida gani basi? Tunaona katika makanisa yetu, wanawake waliokata nywele zao, wanaovaa kaptura, rangi, vipodozi, tunawaona wanaume wenye mfupa wa shingo ya kuku badala ya uti wa mgongo, tunaona wahubiri mimbarani bila nguvu za kutosha ku—kuvunja yai, na kisha wanajiita wahubiri. Jambo ni kwamba, ndugu, hawajapokea ile chanjo, hakuna lingine.

132 Mnajua, ukichukua fomula ya daktari, nawe uanze kuivuruga, utamwua mgonjwa wako. Hiyo ni kweli. Lakini shida yetu ni nini, ni bingwatapeli fulani muuza dawa kutoka kwenye seminari fulani amejaribu kuchanganya fomula hii na kupeana mikono, na lundo zaidi la upuuzi. Hiyo ndiyo sababu wana kanisa lililokufa tulilo nalo siku hizi. Limeuawa kwa sababu hawakufuata fomula ya maagizo.

Kasema, "Haileti tofauti yoyote."

133 Paulo alisema ilileta, alisema, "Kama Malaika kutoka Mbinguni akiwahubiri ninyi injili nyingine yoyote, na alaaniwe." Wana washiriki wa kanisa waliokufa kwa sababu wanajaribu kujipumbaza na agizo hilo, kupeana mikono, kunyunyizia, aina zingine zote, na chochote kile. Fuata yale maagizo yanayosema hasa. Kama ukinywa baadhi ya hivyo viuasumu, utamwua mgonjwa, kama ukiweka viuasumu vingi kupita kiasi, huyo mwuaji humo ndani hataua huo ugonjwa, inywe jinsi tu ilivyoandikwa. Amina. Haleluya! Ninaamini ni kweli kwa moyo wangu wote. Bila shaka.

134 "Je, hakuna zeri katika Gileadi? Hivi hakuna tabibu hapo? Basi ni kwa nini binti ya watu Wangu yuko na ugonjwa wa upungufu wa damu, alivyo usiku wa leo?" Ni kwa nini, Kanisa liko katika hali liliyomo usiku wa leo? Kwa sababu walijipumbaza na yale maagizo. Naam, kuna Zeri katika Gileadi. Haleluya! Kuna Zeri pale. Kristo yupo. Yeye ndiye ile Zeri. Dungweni Uzima Wake.

135 Yeye yuko hapa sasa, anatembea miongoni mwetu. Tunamwona akitenda kazi, akifanya ishara na maajabu miongoni mwetu. Kuna Zeri katika Gileadi, na kuna madaktari hapa. Amina. Tunao madaktari. Basi kuna shida gani? Ni ninyi wagonjwa ambao hamtakuja na kukabiliana na ukweli wake, na kufuata ile fomula.

136 Labda nilisema ya kutosha. Roho Mtakatifu na aseme yaliyosalia. "Je, hakuna zeri katika Gileadi? Hivi hakuna tabibu huko? Basi kwa nini Kanisa Langu liko katika hali liliyomo usiku wa leo?" Kuna kasoro mahali fulani. Hiyo ni kweli. Nafikiri tumechukua mafundisho mengi ya sharti badala ya kuyachukua yale maagizo, seminari za kitapeli zikitoa maagizo ya bandia ambayo ni kinyume na maagizo ya asili.

137 Rudini, hiyo ndiyo njia ya kuipata, hayo ndiyo maagizo ya Milele, si kupeana mkono, na ninii . . . kukariri kanuni ya imani, na kitu kama *hiki*. "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu," akasema, "katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie," wa mataifa yote, nyakati zote, wa sehemu zote, kila mahali.

138 "Je, hakuna zeri katika Gileadi? Hivi hakuna tabibu huko?" Kuna Zeri nyingi hapa, kuna sumu nyingi, iko mbele yako. Naam. Kuna shida gani? Ni kwa sababu watu hawataki kuyapokea hayo maagizo, wana madaktari hapa wanaoweza kuyaandika, tayari yameandikwa. Haikubidi kuyaandika tena, tayari yameandikwa, sema tu yale ambayo tayari yameandikwa, kisha uyachukue namna hiyo.

139 Si kupeana mikono kudogo kwa dondoadume, kudogo, kusema, "Nitakariri kanuni ya imani, kanuni ya Imani ya Mitume. Nitakariri 'Salamu, Mariamu' mara moja moja, niwashe mshumaa.'" Upuuzi, tubu la sivyo utaangamia. Sio, "Nitaamini, na kukubali na kuamini." Ibilisi anaamini pia, hilo halikufanyi kuokoka. Lakini huna budi kuzaliwa mara ya pili. Kama umezaliwa mara ya pili, umezaliwa kwa Neno la Mungu, maana Yeye ni Neno nalo Neno liko ndani yako, nalo huitikia kila sentensi kwa "Amina." Amina.

Na tuombe.

140 Baba wa Mbinguni, kuna Zeri katika Gileadi, ninashukuru sana kwa ajili Yake. Ninashukuru sana kuna matabibu ambao hawangechanganya maagizo hayo kwa vyovyote, si kuwaleta washiriki kanisani, bali kuwaleta watoto kwa Mungu, wanadumu nayo. Si kupeana mikono baridi, kanuni ya imani ama chochote kile, bali maagizo halisi, yaliyoandikwa na Mungu Baba, Mwenyewe, na kutolewa kwa ajili ya maagizo ya Milele. Baba Mungu, yeye alisema ilikuwa ni kwa ajili ya watoto wao, na wale walio mbali, Mataifa, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie wangeweza kumpokea Roho Mtakatifu. Sisi hawa hapa katika Nuru za jioni usiku wa leo.

141 Huko nyuma kabisa hapo mwanzo, kabla ulimwengu haujaumbwa, ulikuwa nao niani Mwako, na hapo lilikuwa wazo, kisha likatamkwa, na ndipo usemi huo ukawa halisi. Na sasa, Mungu, uliandika majina yetu kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

142 Na, Baba Mungu, ninaomba usiku wa leo, kama kuna yeyote wa Mbegu hiyo aliye hapa, katika kanisa hili usiku wa leo, mimi si Hakimu, Wewe ndiwe, mimi ninawajibika tu kwa kuhubiri Neno Lako, lakini kama kuna yeyote wa Mbegu hiyo hapa usiku wa leo, Bwana, nami ninaamini ya kwamba Nuru hiyo itaiangazia, hana budi kupata Uzima. Ataiona hakika kabisa, kwa maana amechaguliwa tangu zamani kuiona, hana budi kuiona.

143 Bwana, Wewe ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Wote alionipa Baba watakuja." Bwana, je, wako hapa usiku wa leo, ambao umepewa Wewe? Kama ndivyo, ninaomba ya kwamba wataiona ile Nuru na kutembea ndani Yake, watubu dhambi zao. Tujalie, Bwana.

144 Si kuchukua kibadala na kuona maishani mwao, wengi wa watu hawa wanaokiri kwamba wameipokea, na angalia jinsi wafanyavyo, pia angalia jinsi wanavyotenda, na kulipuuza Neno, na kuondoka na kusema siku za miujiza zimepita. Wanawake wetu wanaanza kuwa wa kawaida kama walimwengu wengine. Mungu, nimekuwa nikiwaonea wivu. Na—naomba ya kwamba Wewe utawafanyia jambo fulani. Tujalie, Bwana.

145 Loo, rudini Kalvari, enyi watu, rudini kwenye yale maagizo, rudini mkatubu na mfe kwa nafsi zenu, na mwokolewe na kujazwa na Roho Mtakatifu.

146 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, na mioyo yetu imeinamishwa, utu wetu wa ndani kabisa umeinamishwa, na Neno la Mungu likiwa mbele zetu, je, mngehitaji maombi? Nitawaomba tu mwinue mikono yenu. Mseme tu, "Ninainua mkono wangu." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Vema.

147 Sasa, jamani, mimi sikosoi, bali mimi. . .Roho Mtakatifu yuko juu yangu, nami ninataka kusema hivi: Mimi si mmoja wa hawa wahubiri hapa ambao watazunguka, wakitaka. . .

Watu siku hizi wanataka kuburudishwa, wanataka kupata puto la hela, "Sasa, simama. Hatua nyingine, fanya *hivi*, hatua inayofuata fanya *vile*."

148 Nina hatua moja tu, hiyo ni kutubu, na inayofuata ni kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, halafu jambo linalofuata, Mungu alisema, "Nitawapa Roho Mtakatifu." Hizo ndizo hatua tatu ninazojua kuchukua. Sina maputo ya hela, wala sina pini za dhahabu za kuwapa mpate kuhudhuria shule ya Jumapili, ninayo Injili. Ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye.

149 Sasa, kama wewe ni Mkristo anayeparuza, kama wewe ni mtumishi halisi wa Kristo, ninazo, usiku wa leo, baraka kwa ajili ya watu, ninayo karama itakayofanya kazi miongoni mwa watu ambayo ni thibitisho kwamba nimewaambia ukweli. Mnafikiri Mungu Baba, angewahi kumtuma mnafiki ama u—u—ujumbe wa bandia, kisha ageuke na kuthibitisha ujumbe huo? Huyo siye Mungu wetu. Mungu wetu ni safi, asiyeghoshiwa, na mtakatifu. Hana uhusiano wowote na makosa. Yeye ni Kweli, Naye hudumu kwa Neno Lake, Yeye ni Neno.

150 Sasa, hebu wagonjwa waangalie huku na kuamini. Mimi si mponyaji, mimi ni ndugu yenu. Wewe amini, uone kama hiyo chanjo ni sahihi, uone kama yale aliyosema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," Yohana 14:12.

151 Huyu mama aliyeketi kwenye mstari wa mbele hapa, mwanamke mjane, anamwombea mwanawe. Unaamini ya kwamba Mungu atakutimizia haja? Mlevi sugu, hunywa pombe. Unaamini Mungu atalishughulikia? Je, una kadi ya maombi? Huna. Huhitaji moja. Kama utaamini kwa moyo wako wote, itamwacha.

Sasa, simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona, bali Mungu anamjua. Kweli. Mungu ni Mungu. Amina.

152 Yule mwanamke anayeketi moja kwa moja kule nyuma, akimwombea mumewe, amevaa nguo ya madoadoa. Kama ataamini kwa moyo wake wote, Mungu atamjalia haja yake, kama tu ataamini kabisa. Mungu akubariki.

153 Simjui mwanamke huyo. Hahitaji kadi yoyote ya maombi. Wewe, una moja? Huna. Una kadi ya maombi. Unayo? Vema, haikubidi kuitumia, haikubidi kuingia mstarini. Kamwe usishuku yale umesema . . . yale uliyoambiwa kwamba ni kweli, nawe unaweza kupata ulichosema. Amina.

154 Amina. Loo, nina furaha sana kwa ajili ya chanjo ya kutoka kwa kutokuamini! Dhambi ni nini? Kutokuamini. "Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa," hawezi hata kufikia hatua ya kwanza. Uko nje ya mchezo kwa jumla, ulitolewa nje hata kabla hujafika kwenye sahani. Huna budi kuamini kila Neno la Mungu. Yesu alisema, "Kazi nizifanyazo . . . Kama ninii

Yangu. . .” Kama Roho wa Mungu anakaa ndani yako, hivi hatatoa Uhai ule ule uliokuwa ndani Yake? Hakika, atatoa.

155 Maskini mwanamke aliyeketi hapo akiwa na shida hiyo ya titi lake, kama ataamini, Mungu atamponya. Unaamini hilo, Mama? Unaamini? Huna kadi ya maombi? Huhitaji moja kama utaamini. Uvimbe huo utapungua, utakuwa mzima na mwenye afya. Utaamini? Vema.

156 Huyu hapa ameketi mwanamke, ameketi hapa ameinamisha kichwa chake, akiomba. Huyo mwanamke atakufa Mungu asipomsaidia. Hatoki hapa. Ulikuwa na imani zaidi ya ulivyodhania ulikuwa nayo. Umetoka huko chini karibu na Santa Anna. Una kansa, ukiketi kwenye kiti-. . .umefanyiwa upasuaji kwa ajili yake. Je, una kadi ya maombi? Huna. Huhitaji moja. Una kansa, imerudi. Mungu atakuponya.

157 Sikiliza, mtu fulani alikuleta hapa usiku wa leo, aliyekuwa hapa jana usiku naye alikuwa na imani ya kutosha kuitwa kutoka mstarini na kuponywa ugonjwa wa moyo, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hili hapa jambo lingine ninaloona, wewe ni mwanamke mhubiri. Hiyo ni kweli. Sasa, kama unamwamini Mungu wala hutakuwa na shaka moyoni mwako, utaendelea na ujumbe wako. Naam. Wewe amini tu.

158 Kama ningekuwa mahali pako, ninaamini ningesimama kutoka kwenye kiti hicho, na kutoka nje ya jengo hili, na kumwamini Mungu. . .Utakufa ukiketi hapo, kwa hiyo ningetoka kwenye kiti hicho, na kwenda nikimwamini Mungu, na niende nipate afya. Utakufa ukiketi hapo, madaktari hawawezi kukufanyia chochote, tayari wamejaribu.

159 Kama vile yule mwenye ukoma aliyeketi langoni alivyosema, “Kwa nini tuketi hapa mpaka tufe?” Kama wakienda mjini, huko Samaria tayari walikuwa wanakufa kwa njaa, wakila watoto wa mmoja kwa mwenzake, kama waliketi pale walikufa, iliwabidi kushuka kwenda kwenye kambi ya adui. Nao wakachukua nafasi hiyo.

160 Haikubidi kubahatisha, hujaalikwa kwenye kambi ya adui, umealikwa kwenye Kiti cha Enzi cha Baba yako anayekutarajia uje usiku wa leo. Kama una imani ya kutosha kugusa upindo wa vazi la Yesu Kristo, kwamba angeitumia sauti yangu kukujibu, basi huna. . .shikilia imani hiyo na uondoke hapa na uwe mzima, kama utaamini. Utafanya hivyo? Amina.

161 Ninampa changamoto kila mtu hapa ndani kuamini hiyo chanjo. Mnaiamini? Ninyi nyote mnaiamini hiyo? Basi simameni kwa miguu yenu na kupokea uponyaji wenu katika Jina la Yesu Kristo. (Njoo huku, Ndugu.) Hiyo ni kweli. Loo, amina!

Chukua kiti chako na ukisukume uende nyumbani.

Huyo hapo, ametoka kwenye kile kiti, akienda kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Mnaamini? Utukufu!

162 Sasa, hivi hamwoni Yeye yupo hapa? Ile chanjo, ile Zeri iko hapa. Utukufu kwa Mungu! Liaminini marafiki, msiogope kumwamini Yeye. Haleluya! Imani yenu iko wapi?

163 Unajisikia tofauti, sivyo, Dada? Unaweza kuchukua maskini kiti chako cha magurudumu sasa na uende nyumbani na uwe mzima. Chukua . . . Usitie shaka, usitie shaka, dumisha tu imani iyo hiyo uliyo nayo. Kama una ya kutosha . . . Unajua mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, vema, ulifanya jambo lile lile, basi nenda ukaamini.

> Nitamsifu, nitamsifu.
> Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;

Hebu tuuimbe, kila mtu, tuinue mikono yetu.

> Nitamsifu, nitamsifu,
> Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
> Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
> Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila . . .

Vema, ninyi nyote mlioinua mikono yenu kwa ajili ya wokovu, njoni mbele sasa tunapoimba tena.

> Nitamsifu . . .

Njoo moja kwa moja sasa.

> . . . nitamsifu,
> Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
> Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
> Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila . . .

164 Hivi hujawahi kuyachukua yale maagizo? Hivi hujawahi kuchanjwa, hujawahi kujaribu yale maagizo, hujawahi kujazwa na Roho Mtakatifu? Mbona usije sasa? Hili ndilo. Mungu huthibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa. Kuna Zeri katika Gileadi, kuna Zeri, kuna matabibu. Kwa nini usije wakati tukiuimba tena?

> Nitamsifu, ni . . .

Kama unataka Roho Mtakatifu, njoo.

> Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
> Loo, mpeni . . .

165 Bwana Yesu, tujalie haja hizi. Wape afya katika Jina la Yesu. Amina.

> . . . watu,
> Kwa kuwa Damu Yake imeosha . . .

Njoni, kila mtu aje moja kwa moja, ninyi nyote mnaomhitaji Kristo.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha . . .

166 Njoni, maji yametibuliwa. Ingieni ndani, kila mtu, mnapoweza. Wakati maji yametibuliwa, njoni.

Nitamsifu, nitasifu . . .

Kama una haja ya Mungu, njoo.

. . . Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni . . . watu,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Nitamsifu, nitamsifu,
Msifuni Mwana-Kondoo kwa ajili ya mwenye dhambi . . .

Hivi hutakuja sasa, kabla haijachelewa sana?

Loo, mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila doa.

Nitamsifu, nitamsifu . . . (Gusa—mguse Yeye.),
Msifuni Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya wenye dhambi;
Mpeni utukufu enyi watu wote,
Kwa kuwa Damu Yake imeosha kila . . .

Na tuinue mikono yetu sasa na kumsifu.

Nitamsifu . . .

62-0622E Kwa Nini?
Great Western Exhibit Center
South Gate, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org